

OFISI YA KUTAFUTIA WAKIMBIZI MAKAZI MAPYA

Kituo cha Kupiga Simu cha Kitaifa

LAINI YA KUPATA USAIDIZI: Piga simu au tuma ujumbe 1 (800) 203-7001 |

Barua pepe: information@ORRNCC.com

WATOTO

Ikiwa uko katika hali hatari, piga simu kwa 9-1-1

Ikiwa unakabiliwa na matatizo ya afya ya akili, piga simu kwa 9-8-8

Ikiwa unakabili mojawapo ya yafuatayo, tuko hapa kukusaidia:

- Huna mahali pa kulala
- Mtu anakulazimisha kufanya jambo linalokutia wasiwasi
- Mtu fulani anakunyima chakula, makazi, elimu, au dawa
- Ni vigumu kwako kuhisi salama na furaha
- Una hasira au unaumia
- Unahisi huzuni sana au unahisi hukubaliki
- Matatizo ya kifamilia
- Watoto kuwa wakatili kwako shuleni
- Ugumu kupata msaada
- Matatizo na mahakama
- Tatizo la kupata stakabadhi yako

Kwa Wazazi na Wafadhili

Je, unatafuta mtoto anayekuja Marekani?

- Tutahakikisha kwamba ujumbe wako unafika kwenye makao yanayomtunza mtoto wako



Tunafungua masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Nambari za Kimataifa:

- Guatemala - 50218003750042
- El Salvador - 5038006439
- Honduras - 50480027916001
- Mexico - 528008770404

Je, mtoto wako tayari yuko nyumbani?

Tunaweza kusaidia na:

- Kutafuta rasilimali katika jamii yako kwa ajili ya elimu, matibabu, usaidizi wa kihisia, haki ya watoto, matumizi ya dawa za kulevya, usaidizi wa kisheria na usalama.
- Usaidizi wa masuala ya tabia ya mtoto baada ya kuunganishwa, ikijumuisha:
 - Watoto kutoroka
 - Watoto wakihisi huzuni nyingi au hasira
 - Kujihusisha na dawa za kulevya au magenge
 - Mahusiano yasiyofaa
 - Watoto kuwaumiza watoto wengine
 - Watoto kuingia katika matatizo shuleni
 - Tabia yoyote inayokutia wasiwasi
- Kukutegemeza ili kusaidia kuimarisha uhusiano wako na mtoto wako
- Usaidizi wa kuhakikisha mtoto wako anaenda shule na kupata elimu
- Msaada kwa ajili ya matatizo ya kifamilia au dhuluma nyumbani
- Msaada wa kupata nakala za rekodi za mtoto/chanjo na kujaza stakabadhi
- Usaidizi wa kupata utegemezo wa kisheria na kuelewa taratibu za mahakama



1 (800) 203-7001

WhatsApp

- (800) 203-7001

Ujumbe mfupi

- (800) 203-7001



ORR National Call Center
& Sexual Abuse Hotline